JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

## TAARIFA KWA UMMA

# MWALIKO WA MAOMBI MAPYA NA UPANDISHAJI DARAJA WA LESENI ZA MAUDHUI YA REDIO ZA FM

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na.12 ya mwaka 2003 yenye jukumu la kusimamia huduma za mawasiliano ya Kielektroni na Posta nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa Kanuni za Taratibu za Utoaji Leseni, Tangazo la Serikali Na.422 la mwaka 2014, TCRA imeainisha Masafa kwa ajili ya utoaji wa Huduma za Maudhui kwa njia ya redio za utangazaji za FM. Hivyo dirisha la maombi ya leseni ya utoaji wa huduma za maudhui kwa njia ya redio za utangazaji za FM limefunguliwa katika maeneo yafuatayo:-

| NA | MKOA | ENEO LA HUDUMA | IDADI YA MASAFA YA FM YALIYOPO |
|---|---|---|---|
| 1. | Njombe | Njombe<br>Ludewa<br>Wanging'ombe<br>Makete<br>Makambako | **22** |
| 2. | Kilimanjaro | Moshi<br>Hai<br>Rombo<br>Same<br>Mwanga<br>Siha<br>Moshi Vijijini | **2** |
| 3. | Kigoma | Buhigwe<br>Kigoma<br>Kasulu<br>Kibondo<br>Uvinza<br>Kakonko | **6** |
| 4. | Mtwara | Newala<br>Nanyumbu<br>Tandahimba | **12** |

| NA | MKOA | ENEO LA HUDUMA | IDADI YA MASAFA YA FM YALIYOPO |
|---|---|---|---|
| 5. | Simiyu | Bariadi<br>Busega<br>Itilima<br>Maswa<br>Meatu | **25** |
| 6. | Singida | Singida<br>Manyoni<br>Ikungi<br>Mkalama<br>Iramba | **15** |
| 7. | Rukwa | Sumbawanga<br>Sumbawanga Vijijini<br>Kalambo<br>Nkasi | **25** |
| 8. | Manyara | Hanang<br>Kiteto<br>Mbulu<br>Simanjiro<br>Babati | **11** |
| 9. | Ruvuma | Mbinga<br>Nyasa<br>Tunduru<br>Songea<br>Namtumbo<br>Madaba | **15** |
| 10. | Lindi | Lindi<br>Kilwa<br>Mtama<br>Liwale<br>Ruangwa | **18** |
| | Masasi na Nachingwea | Masasi<br>Nachingwea | **25** |
| 11. | Mara | Musoma<br>Rorya<br>Serengeti<br>Tarime<br>Butiama<br>Bunda | **14** |
| 12. | Iringa | Iringa<br>Kilolo<br>Mafinga<br>Mufindi | **9** |

| NA | MKOA | ENEO LA HUDUMA | IDADI YA MASAFA YA FM YALIYOPO |
|---|---|---|---|
| | | Iringa Vijijini | |
| 13. | Shinyanga | Shinyanga<br>Kahama<br>Kishapu | 2 |
| | | Msalala | 1 |
| | | Ushetu | 1 |
| 14. | Tabora | Tabora<br>Igunga<br>Kaliua<br>Urambo<br>Nzega<br>Uyui<br>Sikonge | 11 |
| 15. | Kagera | Karagwe<br>Misenyi<br>Kyerwa<br>Ngara | 3 |
| 16. | Katavi | Mpanda<br>Nsimbo<br>Tanganyika<br>Mlele<br>Mpimbwe | 25 |

Waombaji wanatakiwa kuzingatia Mwongozo wa uwasilishaji wa maombi unaopatikana katika tovuti ya TCRA: www.tcra.go.tz.

Maombi yote ya utoaji wa huduma tajwa hapo juu yawasilishwe kwa kupitia mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao Tanzanite Portal kupitia kiunganishi kifuatacho: https://tanzanite.tcra.go.tz/index.htm kabla ama ifikapo tarehe 24 Oktoba, 2026

Imetolewa tarehe **27 Agosti, 2026**

Digitally Signed By
PETER PHILLIP MWASALYANDA
Thu Aug 27 18:14:44 EAT 2026

Mhandisi Peter P. Mwasalyanda
**MKURUGENZI MKUU**

# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA







**MWONGOZO WA UWASILISHAJI MAOMBI YA LESENI ZA MAUDHUI YA UTANGAZAJI (UTANGAZAJI WA BIASHARA – RADIO) KUPITIA MWALIKO WA MAOMBI (ITA)**

**Agosti, 2026**

## 1. UTANGULIZI

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Na.12 ya 2003 yenye jukumu la kusimamia sekta ya mawasiliano ya kielektroniki na posta katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na huduma za utangazaji Tanzania Bara. TCRA inatoa mwongozo huu wa maombi ya leseni za maudhui ya utangazaji wa redio (Utangazaji wa Biashara) na uwasilishaji wa maombi hayo kwa njia ya mwaliko (Invitation to Apply – ITA).

Maombi yote ya leseni yanafanyika mtandaoni kupitia mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao *Tanzanite Portal* kupitia kiunganishi kifuatacho: https://tanzanite.tcra.go.tz/login.htm.

## 2. SIFA ZA MWOMBAJI WA LESENI

a) Mwombaji anatakiwa awe ni Kampuni iliyosajiliwa na BRELA au Taasisi/Shirika/Asasi ambayo imesajiliwa na vyombo husika vya usajili.
b) Waombaji ambao tayari wana Leseni za Utangazaji wa redio wanatakiwa wawe wamekamilisha malipo yote ya ada za leseni na wahakikishe wana leseni hai kabla ya kufanya maombi mapya.

## 3. UTARATIBU WA MAOMBI YA LESENI BINAFSI

a) Mwombaji yeyote wa leseni atafungua akaunti katika mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao Tanzanite Portal kupitia kiunganishi: https://tanzanite.tcra.go.tz/login.htm
b) Mwombaji anahitajika kuandaa taarifa au nyaraka zifuatazo ili kupakiwa kwenye mfumo: -

**A. Taarifa muhimu za taasisi**

i) Nakala iliyoidhinishwa ya nyaraka za usajili kwa Kampuni (Memorandum and Articles of Association) au Katiba kwa Mashirika au Asasi zisizo za Kiserikali (Certified copy of Memorandum and Articles of Association or constitution for registered societies and NGOs);
Zingatia sharti la umiliki wa hisa kwa mujibu wa Kanuni ya 22 (1) (b) ya Kanuni za Leseni za Mwaka 2018 *inayomtaka Mwombaji Leseni ya Maudhui kuwasilisha nyaraka za Kampuni inayoonesha Kampuni inayoomba Leseni inamilikwa na Mtanzania kwa asilimia zisizopungua hamsini na moja*.
ii) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha Usajili wa Jina la kituo;
iii) Nakala ya cheti cha Usajili kwa kampuni zilizosajiliwa;
iv) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha Usajili kwa vyama au mashirika yaliyosajiliwa;
v) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha Wadhamini Waliosajiliwa (Majina ya wadhamini yaambatishwe);
vi) Nakala ya cheti cha Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN);
vii) Nakala ya hati safi ya kodi (Tax clearence Certificate) inayotumwa kwenda TCRA;
viii) Uthibitisho wa uraia wa wanahisa (Pasipoti, Cheti cha Kuzaliwa, au Kitambulisho cha Taifa); na

ix) Tovuti na anwani za baruapepe (Zingatia: Usajili wa Majina ya Vikoa ni lazima uwe umetumia msimbo wa nchi (dot tz country code top level domain – ccTLD).

**B. Mpango wa Biashara**

Mpango Mahsusi wa biashara (Business Plan) unapaswa kujumuisha maudhui/nyaraka zifuatazo;

i) Wasifu wa Kampuni au Taasisi (Company Profile);
ii) Muhtasari wa malengo, maono na dhamira ya kuanzishwa kwa mradi wa utangazaji;
iii) Miongozo, vipeperushi na maelezo ya kiufundi ya vifaa vitakavyotumika;
iv) Ratiba ya utekelezaji wa mradi na mpango wa ujenzi;
v) Taarifa kuhusu rekodi / uzoefu (marejeleo);
vi) Maelezo kuhusu Huduma itakayotolewa;
vii) Muundo wa gharama na bei ya Huduma;
viii) Makadirio ya msingi kuhusu wigo wa wateja;
ix) Mkakati wa maendeleo ya rasilimali watu;
x) Mkakati wa huduma kwa wateja (kuhakikisha ubora wa huduma);
xi) Ujenzi wa kituo, mchoro wa mpangilio, vifaa na viwango vya utangazaji kama inavyoelekezwa na muhtasari katika **Kiambatisho I**;
xii) Sera ya uhariri ya kituo (Kanuni za Maadili ya Kituo) kulingana na kielelezo kilichoidhinishwa na TCRA (kilichoambatishwa kama **Kiambatisho II**) na maudhui yawe kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroni na Posta (Maudhui ya Redio na Televisheni), za 2018;
xiii) Mpango wa kina wa vipindi vya Siku 7 unaotarajiwa ambao unaakisi muundo ulioidhinishwa na TCRA ulioambatishwa kama **Kiambatisho III** cha Muongozo huu kwa kuzingatia sifa zifuatazo. -
    a) Ubora na aina (variety);
    b) Manufaa kwa uchumi wa ndani;
    c) Kupanua uchaguzi wa programu, ikijumuisha programu za watoto kwa mujibu wa mahitaji yaliyotolewa chini ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroni na Posta (Maudhui ya Redio na Televisheni), ya 2018 kwa muda na kiasi (duration and quota); na
    d) Faida na manufaa kwa maendeleo ya sekta ya utangazaji kwa ujumla
xiv) Taratibu za udhibiti wa ubora wa maudhui ya utangazaji;
xv) Muundo wa Shirika au menejimenti;
xvi) Mchanganuo wa fedha zinazotarajiwa kuwekezwa kwenye biashara (mtaji). Mfano **Kiambatisho IV;**
xvii) Makadidirio ya miaka mitano ya Taarifa tatu za fedha: Taarifa ya mapato na matumizi, mtiririko wa fedha na taarifa ya mizania;
xviii) Udhibitisho halali wa uwezo wa kifedha wa fedha zinazotarajiwa kuwekwa kwenye biashara (mtaji) kama ulivyooainishwa kwenye **kiambatisho V (6.2)**

**C. Malipo ya Ada ya Maombi**

Baada ya kupakia kwenye mfumo taarifa zilizoainishwa hapo juu, mwombaji atatakiwa kulipa ada ya maombi kwa kutegemea maombi husika baada ya kupata namba ya malipo kwenye mfumo.

i) Ada ya Maombi ya Sh. 1,600,000 kwa Waombaji Wapya – Aina ya Leseni ya Wilaya;
ii) Ada ya Maombi ya Sh. 1,600,000 kwa Waombaji wanaopanda kutoka kuwa na leseni ya Kiwilaya hadi Kimkoa (upgrade);
iii) Ada ya Maombi ya Sh. 3,200,000 kwa Waombaji wanaopanda kutoka kuwa na leseni ya Kimkoa hadi Kitaifa (upgrade);

Ada ya maombi itatakiwa kulipwa kabla ya dirisha la uombaji wa leseni za maudhui ya utangazaji wa redio (Utangazaji wa Biashara) halijafungwa **tarehe 24, Oktoba 2026**. Maombi yatakayolipiwa baada ya tarehe hiyo hayatafanyiwa kazi na malipo yatakayolipwa hayatarejeshwa.

Pendekezo la biashara pamoja na viambatisho vyake vinavyohusika vitakuwa kwa kifupi na kwa muhtasari vikilenga leseni iliyoombewa, na mada zake zitakuwa kwa mujibu wa Muundo wa Kielezo cha pendekezo la mradi ulioambatishwa pamoja na mwongozo huu kama **Kiambatisho V**.

## 4. ENEO LA HUDUMA LA LESENI

a) Eneo la huduma kwa leseni ya daraja la Kiwilaya (*District licence*) litahusisha eneo moja (1) la huduma ya utangazaji kama ilivyoainishwa kwenye tangazo kwa Umma.
b) Eneo la huduma kwa leseni ya daraja la Kimikoa (*Regional licence*) (Utangazaji wa Redio) litahusisha hadi maeneo kumi (10) ya huduma ya utangazaji kama ilivyoainishwa kwenye tangazo kwa Umma.
c) Eneo la huduma kwa leseni ya daraja la Kitaifa (*National licence*) (Utangazaji wa Redio) litahusisha kuanzia maeneo kumi na moja (11) ya huduma ya utangazaji kama ilivyoainishwa kwenye tangazo kwa Umma.

## 5. TATHMINI YA MAOMBI

a) TCRA itafanya tathmini ya maombi yote kulingana na vigezo vilivyoainishwa katika mwongozo huu kwa kuangalia uwezo wa kiufundi, maudhui, uzoefu wa utoaji huduma za redio na mchanganuo wa kifedha; na ametimiza sifa za mwombaji kama ilivyoelekezwa kwenye Sehemu ya 2 ya mwongozo huu. Vigezo vya tathmini kwa wenye sifa za uombaji wa leseni ni kama ilivyoainishwa kwenye **Kiambatisho VI**.
b) Endapo waombaji waliofuzu katika eneo moja wapo la huduma ni wengi zaidi ya idadi masafa yaliyoainishwa katika eneo husika: -
    i.) ***TCRA itayaingiza masafa hayo katika mchakato wa ushindani yaani zabuni/ Mnada.***
    ii.) Waombaji ambao wataingia kwenye ***mchakato wa ushindani wa zabuni au mnada watajulishwa namna ya kushiriki kupitia muongozo wa mnada utakaotolewa na TCRA***.

**Kiambatisho I**

## MPANGO MAHSUSI WA BIASHARA (BUSINESS PLAN) UNATAKIWA UONESHE

### A. MAHITAJI YA JUMLA YA KITUO CHA UTANGAZAJI KAMA IFUATAVYO

| S/N | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| i. | TAA YA KUONESHA KUWA STUDIO IKO HEWANI | Ni lazima taa ya kuashiria kipindi kinaenda hewani ifungwe kwenye lango la chumba cha studio juu nje na ndani ili kuwataarifu watu kuhusu shughuli zinazofanyika ndani ya studio. |
| ii. | KELELE NA UDHIBITI WA SAUTI NDANI YA CHUMBA CHA STUDIO | Vyumba vya studio lazima vufungwe mfumo maalumu wa kuzuia sauti (kutoka au kuingia studio wakati kipindi kinaendelea) na mwangwi ili kuwezesha usikivu madhubuti usio na mwingiliano wa sauti au mwangwi kwa wasikilizaji. |
| iii. | UDHIBITI JOTO WA CHUMBA NA HEWA | Vyumba vya utangazaji vya studio sharti viwe na hewa ya kutosha na/au vidhibiti joto kwa ajili ya afya na usalama wa watumiaji na uendeshaji bora wa vifaa vya studio (mfano: viyoyozi, n.k.). |
| iv. | VIPIMO VYA CHUMBA CHA MATANGAZO (LIVE) | Chumba cha utangazaji sharti kiwe na eneo lisilopungua mita za mraba 16 (16m$^2$) na urefu wa angalau mita 2.5 kutoka sakafuni hadi darini ili kuwa na nafasi ya kutosha katika uendeshaji wake. |
| v. | VIPIMO VYA CHUMBA CHA UTENGENEZAJI WA VIPINDI | Chumba cha utengenezaji wa vipindi sharti kiwe na eneo lisilopungua mita za mraba 16 (16 m$^2$) na urefu wa angalau mita 2.5 kutoka sakafuni hadi darini ili kuwa na nafasi ya kutosha katika uendeshaji wake. |
| vi. | VIPIMO VYA CHUMBA CHA UANDAAJI NA UTAFUTAJI WA HABARI | Chumba cha uandaaji na utafutaji sharti kiwe na eneo lisilopungua mita za mraba 16 (16 m$^2$) na urefu wa angalau mita 2.5 kutoka sakafuni hadi darini ili kuwa na nafasi ya kutosha katika uendeshaji wake. |
| vii. | VIPIMO VYA CHUMBA CHA MITAMBO | Chumba kufunga mitambo sharti kiwe na eneo lisilopungua mita za mraba 4 (4 m$^2$) na urefu wa angalau mita 2.5 kutoka sakafuni hadi darini ili kuwa na nafasi ya kutosha katika uendeshaji wake. |
| viii. | UMEME MBADALA (POWER BACKUP) | Mfumo wa mbadala wa nishati sharti ufungwe kwenye jengo la studio na mahali pa kurushia matangazo ili kuhakikisha kuwa kituo kinakuwa hewani hata wakati ambapo nishati ya umeme mkubwa inapokata. |
| ix. | HATUA ZA USALAMA DHIDI YA MOTO | Vifaa vya kuzima moto kama vile vizima moto sharti vifungwe kwenye jengo la studio na mahali pa kurushia matangazo |
| x. | MUUNDO WA MNARA | Mnara sharti uwe na vitu vifuatavyo: -<br>a) Alama za rangi nyekundu na nyeupe;<br>b) Taa za tahadhari za ndege/ anga; na<br>c) Kinga dhidi ya umeme na radi. (Earthing and Electrical Protection) |
| xi. | USALAMA | Ni sharti Studio iwe na uzio mzuri na udhibiti wa uingiaji wa kielektroniki umefungwa kwenye chumba cha studio cha 'kurushia matangazo' na vyumba vingine vya studio. Mfano. bayometriki au Mifumo ya Smartcard, n.k. |

### B. MAHITAJI YA KIUNGO CHA TRANSMITA YA UTANGAZAJI

| NA. | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| i. | ENEO LA UFUNGAJI | Transmita ya STL sharti ifungwe kwenye chumba cha kudhibiti/mitambo (control room) katika studio ya utangazaji, na kipokeaji cha STL kifungwe kwenye eneo la kurushia matangazo (transmitter site) |

| S/N | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| ii. | NJIA ZA KUUNGANISHA STUDIO NA MTAMBO WA KURUSHIA MATANGAZO | Njia za kuunganisha studio na mtambo wa kurushia matangazo ni sharti kutumia kiungo cha pointi kwa pointi (P2P) masafa ya (Microwave), mkongo wa mawasiliano, Kiungo cha IP, n.k. |

**C. MAHITAJI YA MFUMO WA UTANGAZAJI**

| NA. | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| i. | CHUMBA CHA KURUSHIA MATANGAZO (TRANSMITTER ROOM) | Chumba cha kurushia matangazo sharti kiwe na hewa ya kutosha ili kutunza vifaa vya utangazaji na kipokezi cha STL. |
| ii. | NGUVU YA USAMBAZAJI (TRANSMITTING POWER) | Ni sharti kurekebisha nguvu ya usambazaji wa matangazo ili kuepuka mwingiliano na vituo vingine vya redio na isizidi kipimo cha ERP kwa kiasi cha 10KW. |
| iii. | WIGO WA MASAFA | Transmita ya matangazo ya FM sharti ifanye kazi ndani ya bendi ya masafa ya 87.5 MHz hadi 108 MHz. Ni sharti transmita irekebike ili kukubali masafa yoyote yaliyokabidhiwa kwenye masafa yatakavotolewa na TCRA. |
| iv. | ENEO LA URUSHAJI MATANGAZO | Eneo la mnara wa matangazo sharti liidhinishwe na TCRA. Jina la eneo na jira nukta (geographical coordinates) lazima vifafanuliwe vyema. |

**D. MAHITAJI YA VIFAA VYA STUDIO**

| NA. | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| i. | VIFAA VYA VYUMBA VYA MATANGAZO VYA STUDIO | Chumba cha studio sharti kiwe na vifaa vitakavyotumika katika huduma za Utangazaji. Vifaa hivyo ni pamoja na: -<br>a) Kichanganyaji Kitaalamu (Kichanganyaji kilichoteuliwa kwa ajili ya utangazaji wa redio) - *Professional Mixer/Audio Console/ radio panel/ sound panel, or sound desk (Mixer designated for radio broadcasting;*<br>b) Vipaza sauti (kimoja kwa kila Mtangazaji au mwenyeji na chache kwa ajili ya mgeni ikilazimu) - *Microphones (One for each Presenter or host and few for a guest if required)*;<br>c) Mvumo wa kipaza sauti au mkono au stendi - *Microphone boom or arm or stands*;<br>d) Vipokea sauti vya masikioni (Moja kwa kila Mtangazaji au mwenyeji na vingine kwa ajili ya mgeni ikilazimu - *Headphones (One for each Presenter or host and few for a guest if required);*<br>*e)* Kitafuta sauti cha FM (Kipokezi Kimezimwa) - *FM tuner (Off Air Receiver);*<br>*f)* Kiwambo cha spika - *Monitor speaker;*<br>g) Taa ya hewani iliyounganishwa na kudhibitiwa na Meza ya mixer - *On-air light Connected to and controlled by the Mixer Console*;<br>h) Kompyuta iliyofungiwa programu ya Playout na Automation;<br>i) Mseto wa simu - *Telephone hybrid*;<br>*j)* Mfumo wa simu wa kuruhusu kuongea tena (Si lazima) - *Phone Talkback system (Si lazima);*<br>k) Intercom (Si lazima);<br>l) Spika za *Cue/preview* (Si lazima); na |

| | | |
|---|---|---|
| | | m) Mita za Kiwango (Si lazima)- *Level Meter.* |
| ii. | CHUMBA CHA STUDIO CHA UANDAAJI WA MATANGAZO YA REDIO – (*RADIO PRODUCTION STUDIO ROOM)* | Chumba cha studio cha uandaaji wa matangazo ya redio kinaweza kutumika kama chumba cha akiba hewani na lazima kiwe na vifaa vinavyoweza kutumika katika huduma za utangazaji. Mahitaji yake ni kama ya chumba cha utangazaji. |
| iii. | VIFAA VYA CHUMBA CHA UDHIBITI/MITAMBO (*CONTROL ROOM EQUIPMENT)* | Chumba cha kudhibiti/mitambo lazima kiwe na vifaa vitakavyotumika katika kuchakata Mawimbi ya FM kabla ya kusambazwa. Vifaa hivyo ni pamoja na:-<br>a) Seva ya Maudhui ya Matangazo - *Broadcast Content Server;*<br>b) Kiungo cha Studio kwenda kwenye Mtambo wa urushaji matangazo - *Studio to Transmitter Link (STL);*<br>c) Kichanganuzi cha FM - *Modulation monitor/FM analyser*; na<br>d) Jenereta ya FM stereo. |
| iv. | CHUMBA CHA HABARI/CHUMBA CHA KUHARIRI NA MAKTABA | Chumba cha Habari lazima kiwe na vifaa vinavyotumika katika kuhariri na kuhifadhi habari kama vile komputa zilizo na programu tumizi zinazowezesha kuandika habari na kuzihariri, Televisheni, kipokezi cha redio, meza na viti kwa ajili ya wanahabari. |

**E. MAHITAJI YA RASILI MALI WATU KWA AJILI YA KUENDESHA KITUO**

| NA. | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| i. | Idadi ya wafanyakazi wanaokusudiwa kuendesha kituo na elimu zao | Kiwango cha chini cha wafanyikazi<br>Meneja wa kituo - 1;<br>Watozi/Wazalishaji - 1;<br>Waandishi/Wawasilishaji wa Habari - 3;<br>Mhariri - 1; na<br>Fundi - 1. |
| ii. | Elimu ya wafanyakazi | Kiwango cha chini kiwe ni Diploma ya Uandishi Habari au zaidi na cheti kwa mafundi. |

**Kiambatisho II**

**MWONGOZO WA SERA YA UHARIRI**

1. Jina la Kituo………………………………………………………………………

2. Umiliki: Binafsi ☐ Umma ☐

3. Soko: Jumuia ☐ Wilaya ☐ Kimkoa ☐ Kitaifa ☐

4. Aina ya Leseni: Umma ☐ Biashara ☐ Jumuia ☐

5. Maudhui yanayotolewa: -

| | |
|---|---|
| Dini | |
| Elimu | |
| Umma | |
| Biashara | |
| Siyo ya Kibishara | |
| Michezo | |
| Muziki | |
| Nyingine | |

6. Maelezo ya Jumla ya Shabaha ya Sera ya Uhariri ……….................……………
…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
………………………………………

7. Malengo mahususi ya Maudhui Yanayotolewa
……………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

8. Hadhira inayolengwa
…………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
…………………………

9. Matokeo/Mafanikio Yanayotarajiwa
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

10. Mwongozo

| NA. | MWONGOZO | MAELEZO YA MWONGOZO |
|---|---|---|
| 1 | Uadilifu | |
| 2 | Usawa | |
| 3 | Sifa Merit | |
| 4 | Uhuru wa Habari | |
| 5 | Taswira | |
| 6 | Faragha | |
| 7 | Uhuru wa Uhariri | |
| 8 | Kuaminika | |
| 9 | Kutopendelea | |
| 10 | Usahihi | |
| 11 | Mahojiano | |
| 12 | Msambao wa Uchguzi | |
| 13 | Matangazo Mbashara | |
| 14 | Simu zinazoingia | |
| 15 | Uandishi wa Habari za wananchi | |
| 16 | Mitandao ya kijamii kama chanzo cha habari | |
| 17 | Intaneti kama chanzo cha habari | |
| 18 | Vipindi vya Dini | |

| | | |
|---|---|---|
| 19 | Ladha na adabu – *taste and decency* | |
| 20 | Vipindi vya Afya | |
| 21 | VVU na UKIMWI | |
| 22 | Jinsia | |
| 23 | Watoto | |
| 24 | Maudhui kwa hadhira ya watu wazima - *Watershed* | |
| 25 | Uhalifu na Kupinga Shughuli za Kijamii - *Crime and anti Social Activity* | |
| 26 | Mtangazo kuhusu maafa | |
| 27 | Ukatili | |
| 28 | Ripoti kuhusu Vita | |
| 29 | Machafuko, Utekaji nyara na Mateka | |
| 30 | Maonyo ya mabomu | |
| 31 | Maandamano | |
| 32 | Taratibu za Kushughulikia Malalamiko | |
| 33 | Huduma kwa wateja | |

**Msimamo mwingine wowote wa sera za kituo.**

Mimi................................................, Afisa Mtendaji Mkuu wa kituo, ninatamka kwamba taarifa iliyotolewa hapo juu, kulingana na uelewa wangu, ni ya kweli na sahihi.

Ikiwa imetolewa vinginevyo inaweza kuondoa sifa za kituo changu kufikiriwa kupewa Leseni.

**JINA LA AFISA MTENDAJI MKUU WA KITUO:**

**SAINI:**

**TAREHE NA MHURI WA OFISI:**

**Kiambatisho III**

**PROGRAMU INAYOTARAJIWA YA KINA YA SIKU 7**

**[Ingiza siku]**

| Muda | Jina la Kipindi | Lengo mahususi | Hadhira inayolengwa | Mafanikio Yanayotarajiwa |
|---|---|---|---|---|
| 11:00-11:30 | Mfano: Mama na Watoto | Kuielimisha jamii kuhusiana na njia bora ya kuwalea Watoto | Wazazi | Malezi bora |
| 11:30-12:00 | Mfano: Muziki | Kuburudisha | Wote (Vijana na Wazee) | Kuielimisha jamii kuhusu masuala kadhaa kama vile UKIMWI, uhusiano kazini, kwa kutumia nyimbo. |

**[Ingiza siku]**

| Muda | Jina la Kipindi | Lengo mahususi | Hadhira inayolengwa | Mafanikio Yanayotarajiwa |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**Kiambatisho IV**

## MCHANGANUO WA MTAJI

| Na. | Aina | Maelezo | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1. | **Ununuzi na Ufungaji wa Vifaa vya Utangazaji** | Vifaa vya studio, vifaa vya usambazaji wa mawimbi, vifaa vya uchakataji wa sauti, konso za utangazaji, maikrofoni, kamera, seva, mifumo ya ufuatiliaji, miunganisho ya umeme wa dharura, antena, na miundombinu mingine ya kiufundi inayohusiana. | XXXXXX |
| 2. | **Ujenzi wa Studio na Uwekaji wa Miundombinu ya Uendeshaji** | Kazi za ujenzi, ukamilishaji wa ndani, ufungaji wa mifumo ya umeme na mtandao, matibabu ya akustiki na kuzuia sauti, samani na vifaa vya ndani, mifumo ya kiyoyozi na uingizaji hewa, mifumo ya usalama, uunganishaji wa umeme wa dharura, upangaji wa maeneo ya kazi, na miundombinu mingine muhimu. | XXXXXX |
| 3. | **Gharama za Eneo la Usambazaji wa Mawimbi** | Vifaa vya usambazaji wa mawimbi, mifumo ya kupandisha na kushusha mawimbi kupitia satelaiti, antena, minara ya usambazaji wa mawimbi na vifaa vinavyohusiana, miunganisho ya mawasiliano ya microwave au fiber, vifaa vya uchakataji wa mawimbi, mifumo ya ufuatiliaji, na miundombinu mingine ya kiufundi inayohusiana. | XXXXXX |
| 4. | **Uzalishaji wa Maudhui na Shughuli za Uandaaji wa Vipindi** | Upangaji wa vipindi, uundaji wa maudhui, utayarishaji wa habari na masuala ya sasa, vipindi vya burudani na elimu, uandishi wa miswada, uzalishaji wa vipindi studio na maeneo ya nje, uhariri na uchakataji wa maudhui baada ya uzalishaji, ununuzi wa maudhui, upangaji wa ratiba za vipindi, uhakiki wa ubora, na shughuli nyingine muhimu. | XXXXXX |
| 5. | **Uwekaji wa Ofisi na Samani** | Meza za ofisi, viti, makabati, samani za vyumba vya mikutano, vifaa vya mapokezi, vituo vya kazi, rafu, sehemu za kuhifadhia, vifaa vya ofisi, na samani nyingine muhimu. | XXXXXX |
| 6. | **Masoko na Ujenzi wa Chapa** | Uendelezaji wa chapa, kampeni za utangazaji, shughuli za ushirikishaji wa hadhira, uuzaji wa kidijitali, mahusiano ya umma, matangazo, mawasiliano na vyombo vya habari, hafla za uzinduzi, na shughuli nyingine za masoko. | XXXXXX |
| 7. | **Ajira na Mafunzo kwa Watumishi** | Kutangaza nafasi za kazi, michakato ya uteuzi na ajira, utambulisho na uelekezaji wa | XXXXXX |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | watumishi wapya, mafunzo ya kiufundi na kiutendaji, mafunzo kuhusu uzingatiaji wa kanuni na taratibu, mafunzo ya afya na usalama kazini, programu za maendeleo ya kitaaluma, na shughuli nyingine za rasilimali watu. | |
| 8. | **Shughuli za Uendeshaji** | Shughuli za Rasilimali Watu na Utawala, usaidizi wa shughuli za uendeshaji, na gharama za jumla za uendeshaji. | XXXXXX |

**Kiambatisho V**

## MUUNDO WA MAPENDEKEZO YA MRADI KWA AJILI YA MAOMBI YA LESENI

### 1.0 UTANGULIZI:

Maombi ya kituo cha Redio yanapaswa kuambatishwa na muhtasari wa vipengele muhimu (upembuzi yakinifu) ambapo mwombaji (waombaji) ataweza kutoa maelezo ya kina. Vipengele hivi vinaweza kujumuisha: Muhtasari wa kiutendaji, uchambuzi wa soko, masuala ya kiufundi, mfumo wa uongozi, uchambuzi wa kifedha na uwezekano wa mradi.

1.1 **Dira:** Ni kitu gani unachotaka kukifikia kwa kuanzisha Kituo kama hicho cha Redio au Televisheni?

1.2 **Dhamira:** Utafanya nini ili kufikia dira yako?

1.3 **Malengo:** Ni sababu gani zilizoleta msukumo wa kuanzishwa kwa kituo hicho.

1.4 **Eneo:** (mahali halisi) wapi unapanga kuanzisha kituo chako

### 2.0 MCHANGANUO WA SOKO:

2.1 **Hali ya sasa:**

Ni sharti kuwe na maelezo ya hali ya sasa ya utangazaji ya eneo linalohusika unalotaka kuanzisha kituo chako.

2.2 **Kupenya kwa Biashara:**

Je, utawezaje kupenya au kuifikia hadhira unayoihitaji?

2.3 **Makadirio ya Biashara:**

Eleza uendelevu wa biashara yako ndani ya mwaka mmoja au miwili ijayo. Je, utaweza kuendeleza kituo? Jinsi gani?

### 3.0 UCHANGANUZI WA KIUFUNDI:

3.1 Studio na aina/maelezo, mpangilio na eneo ya vifaa vya transmita, Bainisha eneo la transmita za studio.

3.2 Aina za Antena

3.3 Ufungaji na kazi za ujenzi na vifaa (TX/studio)

3.4 Michoro na viambatisho sharti viambatishwe

3.5 Kiungo cha transmita na Studio (STL), mnara wa antena na eneo la litakalofikiwa na mawimbi ya utangazaji *(Coverage area)*

3.6 Kuzingatia uwepo na ubora wa umeme:

- Ugavi wa umeme utakaotumika (Umeme wa TANESCO, Jua, Jenereta n.k)
- Uwezo wa jenereta / UPS na aina zake

- Kidhibiti Umeme (Automatic Voltage Regulator) na uwezo wa vidhibiti umeme (stabiliser capacity)

**4.0 MASUALA YA MAUDHUI:**

4.1 Ratiba ya Vipindi

4.2 Vyanzo vya vipindi

**5.0 MUUNDO WA MENEJIMENTI:**

5.1 Muundo/ chati ya shirika

a) Wasifu wa Kampuni / Taasisi

b) Onesha nafasi ya uongozi, sifa na kazi zao, idadi ya wafanyakazi katika kila sehemu pamoja na viwango vyao vya elimu na utaalam wao.

c) Onesha ajira ya wafanyakazi (Idadi ya wafanyakazi unaotarajia kuwaajiri pamoja na vyeo vyao)

d) Onesha viwango vya juu vya elimu vya wafanyakazi wako muhimu, hii ni kwa meneja wa kituo, msimamizi wa vipindi wahariri, waandishi wa habari na mafundi.

5.2 Maendeleo/Mafunzo ya Wafanyakazi

a) Utatoaje mafunzo kwa wafanyakazi wako?

b) Utajumuishaje teknolojia mpya katika biashara yako?

**6.0 MCHANGANUO WA KIFEDHA:**

6.1 Mchanganuo wa fedha zinazotarajiwa kuwekezwa kwenye biashara (mtaji). Kama ilivyo kwenye mfano wa **Kiambatisho IV**

6.2 Kuthibitisha uwezo wa kifedha wa mwombaji: -Udhibitisho wa uwezo wa kifedha unaweza kuonyesha kupitia;

a) Taarifa ya miezi sita (6) ya benki ya kampuni (bank statement) zilizoidhinishwa na benki husika au Taarifa ya ukaguzi wa hesabu kwa kampuni zinazotoa huduma (audited financial statement) au

b) Taarifa ya miezi sita (6) ya benki (bank statement) za wanahisa kwa kampuni mpya zilizoidhinishwa na benki husika; au

c) Barua ya ufadhili wa mradi kutoka kwa mfadhili ikiambatana na taarifa zake za benki (bank statement) za miezi sita zilizoidhinishwa na benki husika; au

d) Barua kutoka Benki (iliyogongwa muhuri) inayoonyesha kiasi cha mkopo unaoweza kukopesheka.

6.3 Makadirio ya taarifa za fedha ya miaka mitano: Taarifa ya mapato na matumizi (income statement), mtiririko wa fedha (Cashflow statement) na taarifa ya mizania (Balance sheet). Makadirio ya taarifa ya fedha yanapaswa kujumuisha vigezo vya ukokotoaji unaozingatia uwiano ufuatoa: -

(i) Kiwango cha faida halisi (Net Profit Margin)
(ii) Faida kwenye Mtaji wa Uwekezaji (Return on Equity)
(iii) Uwezo wa kampuni kulipa madeni ya muda mfupi (Current Ratio)
(iv) Faida kwenye Uwekezaji (Return on Investment)
(v) Mwenendo wa ukuaji wa mapato kwa miaka 5(Revenue growth)

6.4 Muundo wa gharama na bei ya Huduma;

## 7.0 HUDUMA KWA WATEJA

7.1 Makadirio ya msingi kuhusu wigo wa wateja;

7.2 Mkakati wa huduma kwa wateja (kuhakikisha ubora wa huduma);

## 8.0 HITIMISHO:

Katika hitimisho, sharti mwombaji aeleze **UMUHIMU WA MRADI** yaani manufaa kwa jamii, matarajio ya mapato, fursa za mafunzo ya ajira na jinsi malengo ya kampuni/taasisi yako yatakavyotimizwa.

**Kiambatisho VI**

## VIGEZO VYA TATHMINI YA MAOMBI

### A. Kwa Waombaji Wapya wa huduma za Maudhui ya Redio

| Na. | Kigezo | Alama [%] |
|---|---|---|
| 1. | Uwezo wa kiufundi | 20 |
| 2. | Maudhui (Uanuai (content diversity) na Uzingatiwaji wa Kanuni) | 40 |
| 3. | Idadi na sifa za wafanyakazi muhimu | 15 |
| 4. | Uwezo wa kifedha | 25 |
| **Total** | | **100** |

### B. Kwa Waombaji wa Upandishaji Daraja au kuongeza Maeneo ya huduma za Maudhui ya Redio

| Na. | Kigezo | Alama [%] |
|---|---|---|
| 1. | Uwezo wa kiufundi | 10 |
| 2. | Uzingatiwaji wa Maudhui (Uanuai wa Maudhui na Uzingatiaji wa ratiba) | 30 |
| 3. | Idadi na sifa za wafanyakazi muhimu | 15 |
| 4. | Uwezo wa kifedha | 25 |
| 5. | Uzingatiwaji wa Kanuni na Miongozo | 20 |
| **Total** | | **100** |

**Alama ya chini kwa mwombaji aliyefaulu ni 70%**



## Wasiliana Nasi

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
Mawasiliano Towers, 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S. L. P. 474, Dar Es Salaam
+255 22 2199760 - 9 / +255 22 2412011 - 2 / +255 784558270 - 1
dg@tcra.go.tz | barua@tcra.go.tz